

**HOTUBA YA UFUNGUZI YA MWENYEKITI WA TUME YA
TAIFA YA UCHAGUZI WA MKUTANO WA TUME NA
VIONGOZI WA VYAMA VYA SIASA.**

TAREHE 16 DESEMBA, 2016

Viongozi wa vyama vya Siasa,

Msimamizi wa Uchaguzi wa Mkoa,

Kamanda wa Polisi wa Mkoa,

Wajumbe wa Tume,

Watendaji wa Tume,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote, kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisheni wote kwenye Mkutano huu wa kujadili na kushauriana kuhusu Maandalizi ya Uchaguzi Mdogo wa Mbunge wa Jimbo la Dimani.

Ninatambua kuwa mnayo majukumu mengi yanayowakabili lakini kwa kutambua umuhimu wa Mkutano huu mmeweza kuhudhuria.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kama mnavyojua, Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inasimamia Uchaguzi wa Rais na Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Uchaguzi wa Madiwani kwa Tanzania Bara. Katika utaratibu huo, Tume, baada ya kupokea Taarifa Rasmi ya nafasi wazi za Mbunge jimbo la Dimani, ilipanga Ratiba ya Uchaguzi ambapo tarehe 22 Desemba, 2016 imepangwa kuwa tarehe ya Uteuzi wa Wagombea. Pia Kampeni za Uchaguzi zitaanza tarehe 23 Desemba, 2016 hadi 21 Januari, 2017 na siku ya kupiga kura itakuwa tarehe 22 Januari, 2017.

Ni matarajio ya Tume kuwa, Vyama vya Siasa vitatoa ushirikiano wa hali ya juu ili kuhakikisha Uchaguzi wetu unakuwa huru na wa haki. Lengo hili litafanikiwa tu iwapo

Vyama vinavyoshiriki Uchaguzi na Wagombea wao watazingatia na kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu, Maelekezo ya Tume na Maadili ya Uchaguzi. Tume pia inatumaini kwamba hali hii ya utulivu iliyopo itaendelezwa hadi mwisho wa Kampeni mnamo tarehe 21 Januari, 2016 na Siku ya Uchaguzi tarehe 22 Januari, 2017. Ni matarajio ya Tume kuwa Vyama vya Siasa na Wagombea wataendelea kuelezea kuhusu sera zao na si vinginevyo ili kuepuka matumizi ya lugha ambazo zinaweza kusababisha machafuko.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kila Chama cha Siasa, baada ya kushauriana na Wagombea, kina haki ya kuteua Wakala mmoja kwa kila Kituo cha Kupigia Kura. Ni vyema Mawakala wapangiwe Vituo vya Kupigia Kura ndani ya Shehia wanakoishi ili waweze kuwatambua Wapiga Kura. Vyama vihakikishe kuwa Mawakala wao wanaelewa hatua zote muhimu za Uchaguzi Vituoni kuanzia hatua ya kwanza ya Kufungua Kituo hadi Kutangaza Matokeo. Tume imeandaa Vijiitabu vya Maelekezo kwa Mawakala wa Vyama vya Siasa ili kuwawezesha Mawakala kufahamu wajibu na majukumu yao wanapokuwa

katika Vituo vya Kupigia Kura, Kuhesabu Kura na Kujumlisha matokeo ya Uchaguzi

Kumekuwa na mazoea kwa baadhi ya Vyama vya Siasa kuteua Mawakala wanaotoka Majimbo mengine ya Uchaguzi. Sheria ya Uchaguzi haikukataza jambo hilo lakini Tume inavishauri Vyama vya Siasa kuteua Mawakala wanaotoka ndani ya Jimbo linalofanya Uchaguzi. Aidha, ikumbukwe kuwa Mawakala wa Vyama watagharamiwa na Vyama vyao vya Siasa

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Watu watakaopiga Kura tarehe 22 Januari, 2017 ni wale walioandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. na wana Kadi ya Mpiga Kura. Aidha Vyama viwakumbushe wananchi na mashabiki wao umuhimu wa kila mmoja kutunza Kadi yake na kuepuka kurubuniwa na kukabidhi Kadi zao kwa watu wasiohusika.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Tume inawapongeza ninyi Viongozi wa Vyama vya Siasa kwa kuwa mstari wa mbele katika kuwahamasisha wananchi

kushiriki katika Uchaguzi. Tume ingependa kutumia fursa hii kuwaomba muendeleo kuhamasisha zaidi Wapiga Kura ili wajitokeze kwa wingi Siku ya Kupiga Kura.

Vile vile ni marufuku kwa Mgombea, Chama cha Siasa au Wakala kufanya Kampeni Siku ya Uchaguzi kwani mwisho wa Kupiga kampeni ni siku moja kabla ya Siku ya Uchaguzi yaani tarehe 21 Januari,2016 .

Pia, Tume inawakumbusha kwamba, watu wakishapiga Kura hawapaswi kubaki katika eneo la Vituo vya Kupigia Kura kwa vile wako Mawakala wa Vyama watakaokuwepo Vituoni kusimamia utaratibu wote ikiwa ni pamoja na Upigaji na Uhesabuji wa Kura; na kubandika matokeo nje ya Kituo.

Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,

Kwa kumalizia, napenda kuwashukuru sana kwa kuhudhuria Mkutano huu, na ni matarajio ya Tume kwamba mtachangia kwa kutoa Maoni yenu, au kuuliza maswali yenye tija kwa madhumuni ya kufanikisha Mkutano huu na Uchaguzi kwa ujumla. Tushirikiane wote kwa pamoja ili kuweza kuwa

na Uchaguzi ulio huru na wa haki kwani ndio nguzo muhimu katika kukuza Demokrasia nchini.

Tume inarejea kusisitiza kuwaomba Vyama vya Siasa kuwahimiza Wananchi kwa jumla kutumia haki yenu ya Kikatiba ya kuchagua Viongozi mnaowataka kwa amani na utulivu bila woga au shinikizo lolote kwa kuzingatia tu **Sheria, Taratibu, Kanuni na Maadili ya Uchaguzi** ambayo kila Chama kimekubali na kutia saini.

Baada ya kusema hayo, napenda kutamka rasmi kuwa Mkutano wetu umefunguliwa.

Asanteni Kwa Kunisikiliza